## Utunzaji Maghalani

Utunzaji maghalani unaweza kufanyika katika sehemu yoyote ndani ya jumuiya na bidhaa zinaweza kusafirishwa kwa mfumo mmoja wa dhamana.

## Upitishaji bidhaa (transit)

Mfumo wa upitishaji bidhaa utatumika kwa bidhaa zinazotoka katika nchi ya nje na kuelekea nchi nyingine ya nje kupitia nchi moja au zaidi wanachama wa Jumuiya. Mfumo mmoja wa dhamana utatumika katika upitishaji wa bidhaa.

## Uingizaji bidhaa kwa muda

- Bidhaa zinazoingizwa kwa ajili ya matumizi ya muda ndani ya nchi mwanachama hazitatozwa ushuru wa Forodha;
- Bidhaa zilizoingizwa kwa ajili ya matumizi ya muda zitatumia mfumo wa dhamana wa jumuiya.

## Uhamishaji wa bidhaa kati ya nchi wanachama

Hii inahusisha uhamishaji wa bidhaa zilizokwishalipiwa ushuru kutoka nchi mwanachama.

Pindi ushuru unapolipwa katika nchi mojawapo mwanachama, bidhaa hazitatozwa ushuru wa Forodha pale zinapoingizwa katika nchi nyingine mwanachama.

Bidhaa ambazo awali zilitunzwa ghalani miongoni mwa nchi wanachama zitaingizwa katika nchi mwanachama kwa matumizi ya ndani ya nchi husika.

## Uondoshaji bidhaa kwa ajili ya Nyanda Maalum za Kiuchumi (SEZ), Nyanda za uzalishaji bidhaa za kutoka njen ya nchi (EPZ) na Bandari Huru .

Bidhaa kwa matumizi ya SEZ na EPZ zitaondoshwa kwa dhamana.

## Uhamishaji bidhaa kwa muda

Bidhaa zilizokwishalipiwa ushuru zinazohamishwa kutoka nchi moja mwanachama zitaondoshwa kwa dhamana.

## Mzunguko wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi wanachama.

Bidhaa zinazozalishwa ndani ya jumuiya hazitozwi ushuru wa Forodha zinapohamishwa kwenda nchi mwanachama madamu zimekidhi vigezo vya kanuni za uasili za jumuiya. Bidhaa hizo zinaweza kutozwa kodi za ndani, kama zipo, zinazotozwa katika biashara ya kimataifa pindi zinapoingia ndani ya mipaka ya nchi husika.

## Mzunguko wa bidhaa zilizosamehewa Ushuru

Bidhaa zilizosamehewa ushuru zitaingizwa kwa utunzaji magahalani na zitaondoshwa kwa dhamana.

## Utoaji bidhaa toka nchi wanachama kwenda katika soko nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Uhamishaji wa bidhaa kutoka nchi mwanachama kwa ajili ya kutoa nje ya jumuiya utafanyika kwa kutumia mfumo wa dahamana na utasimamiwa na mfumo wa kielektroniki wa kusimamia mizigo, Electronic Cargo Tracking System (ECTS). Tozo na gaharama zingine za utoaji bidhaa nje ya nchi, kama zipo, zinaweza kutozwa katika nchi mwanachama husika..

**Utendaji katika bandari na mipaka**

Nchi wanachama zisizo na bandari zinaweza kuwa na wawakilishi katika bandari kuu za uingizaji bidhaa.

**Wakala wa Forodha**

Wakala wa Forodha mwenye leseni katika nchi mojawapo mwanachama ataruhusiwa kufanya kazi katika nchi nyingine mwanachama chini ya utambuzi wa pamaoja wa nchi wanachama.


**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Ofisi ya TRA iliyo karibu nawe
AU
Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi,
Mamlaka ya Mapato Tanzania
P.O.Box 11491
Dar es Salaam
Simu Na: 255-22-2119343/2119591-4
Nukushi: +255-22-2128593
Barua pepe: info@tra.go.tz
Tovutu: www.tra.go.tz

Kituo cha Huduma:
0800110016 (TTCL na Vodacom)
0786 800000 (Airtel)
0713 800333 ( Tigo )


EAC
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI



# HIMAYA MOJA YA FORODHA YA EAC



# Utangulizi

Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulisainiwa mwezi wa kumi mwaka 1999, na kuanza kutumika mwezi wa saba mwaka 2000.Kulingana na kipengele namba 5(2) cha mkataba huo washiriki wa jumuiya hii walikubaliana kuwa na umoja katika mambo mbalimbali ambayo ni Umoja wa Forodha, Soko la pamoja, Muungano wa sarafu na hatimaye shirikisho la kisiasa ili kuimarisha uchumi, utamaduni na maendeleo ya kisiasa na muungana kwa faida ya wote.

Protokali iliyoanzisha Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliridhiwa mwaka 2004 na kuanza kutumika rasmi mwezi wa kwanza mwaka 2005.Kuanza kwa Umoja wa Forodha kumekuwa mchakato endelevu na mpaka sasa hatua mbalimbali zimefikiwa kwa lengo la kufikia ukamilifu wa Umoja wa Forodha.

Mwezi wa nne mwaka 2012, mkutano ulijadili ripoti ya baraza la mawaziri kuhusu kufikia Himaya Moja ya Forodha. Ilikubalika kimsingi kuwa mfumo wa sehemu ya kufikia (Destination Model) utumike katika uondoshaji bidhaa wakati ukadiriaji na ukusanyaji wa mapato ufanyike katika sehemu ya kuingilia bidhaa.

## Himaya Moja ya Forodha (SCT) ni nini?

Himaya Moja ya Forodha inaelezwa kama ni hatua mojawapo katika ufikiaji wa Umoja wa Forodha amabao unafikiwa kwa kuondoa vikwazo au kupunguza kiwango cha udhibiti wa mipakani kwa bidhaa zinazotoka ndani ya nchi wanachama na hatimaye kuwezesha mzunguko huru wa bidhaa. Himaya Moja ya Forodha (SCT) inajumuisha nchi wanachama ambao ni Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda.

## Malengo

- Kupunguza gharama za ufanyaji biashara.
- Kuchochea utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) miongoni mwa wanachama na kuboresha ukusanyaji taarifa katika jumuiya.
- Kujenga uwezo na kuboresha mahusiano kati ya sekta binafsi na ile ya umma.
- Kuwezesha utii wa kanuni na taratinu za jumuiya.

## Faida

- Kupunguza gharama za ufanyaji biashara kwa kuondoa milolongo.
- Kupungua kwa gharama za utendaji na usimamizi.
- Kupata manufaa ya kiuchumi na matumizi stahaili ya rasilimali katika uondoshaji wa bidhaa.
- Kuongeza vivutio vya uwekezaji wan je, ndani na ule kati ya nchi wanachama.
- Kuboresha mahusiano kati ya sekta binafsi na ile ya umma.
- Kujenga mfumo wa kuzuia biashara ya magendo katika jumuiya.
- Kupunguza hatari iliyopo kutokana na Kukiuka kwa sheria kwa bidhaa zinazosafirishwa kwenda nchi nyingine.
- Kujenga mfumo madhubuti wa kusimamia mapato.
- Kuwezesha matumizi ya teknolojia ya habari na mwasiliano na ukusanyaji wa takwimu katika jumuiya
- Kuongeza mzunguko wa biashara kutokana na kupungua kwa michakato katika utendaji.
- Kuwezesha Soko la pamoja na kujenga soko moja la ndani.
- Kuondoa vikwazo visivyo vya kodi ili kuwezesha mzunguko huru wa bidhaa ndani ya jumuiya.



## Utendaji wa Himaya Moja ya Forodha (SCT)

Himaya Moja ya Forodha itatekelezwa katika misingi mitatu ambayo ni:

- Mzunguko huru wa bidhaa
- Mifumo ya usimamizi wa Mapato, na
- Mfumo wa kisheria na kitaasisi wa jumuiya

### Mzunguko huru wa bidhaa

Bidhaa za kutoka katika nchi moja mwanachama kwenda nyingine ndani ya Umoja wa Forodha hazitatotzwa Ushuru wa Forodha madamu zimekidhi vigezo vya kanuni za uasili za jumuiya. Bidhaa zilizoingizwa toka nje ya Umoja wa Forodha na kuruhusiwa kwa matumizi ya ndani ya nchi ziko huru kuzunguka ndani ya jumuiya. Kila kundi linahitaji utaratibu wa pekee kulingana na mfumo wa Forodha zilikotolewa tamko.

### Uingizaji bidhaa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

Viwango sawa vya Forodha vitatumika kwa bidhaa zinazoingizwa ndani ya Jumuiya. Bidhaa zinaweza kuwa za matumizi ya ndani ya nchi, utunzaji maghalani au zinzosafirishwa kupitia nchi mwanachama.

## Uondoshaji bidhaa

Uondoshaji wa bidhaa utafanyika katika nchi mzigo unapofika mwisho wakati bidhaa zikiwa katika sehemu ya kwanza ya kuingilia ndani ya jumuiya.